



88132317



International Baccalaureate®  
Baccalauréat International  
Bachillerato Internacional

**SWAHILI B – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SOUAHÉLI B – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SUAHILI B – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Tuesday 12 November 2013 (afternoon)  
Mardi 12 novembre 2013 (après-midi)  
Martes 12 de noviembre de 2013 (tarde)

1 h 30 m

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Section A: choose one task. Each task is worth *[25 marks]*.
- Section B: write a personal response to the stimulus provided. The task is worth *[20 marks]*.
- The maximum mark for this examination paper is *[45 marks]*.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Section A : choisissez une tâche. Chaque tâche vaut *[25 points]*.
- Section B : exprimez votre opinion personnelle sur la réflexion fournie. La tâche vaut *[20 points]*.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est *[45 points]*.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Sección A: elija una tarea. Cada tarea vale *[25 puntos]*.
- Sección B: escriba una opinión personal al estímulo provisto. La tarea vale *[20 puntos]*.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[45 puntos]*.

## **SEHEMU A**

*Kamilisha mojawapo wa kazi zifuatazo. Andika maneno kati ya 250 na 400.*

### **1. Utufauti wa tamaduni**

Wewe ni mwanafunzi katika shule inayoongea Kiswahili na nchi yako imepitisha sheria mpya ambayo inalazimisha vyombo vya habari kupeperusha asilimia hamsini ya vipindi na nyimbo kwa Kiswahili ili kuendeleza utamaduni wenu. Andika makala itakayochapishwa katika gazeti la mwezi la shule ukipinga au kuunga mkono uamuzi huu.

### **2. Mila na desturi**

Likizo iliyopita kulikwa na mashindano ya tamasha ya muziki na michezo ya kuigiza katika nchi mojawapo inayoongea Kiswahili. Katika mashindano hayo, kulikuwa na mengi yanayotambulisha bayana utamaduni wa nchi yako na ukaamua kuandika na kuyaakisi uliyoyaona kwenye blogu yako. Andika hayo katika blogu yako.

### **3. Afya**

Shule yako imeamua kupunguza muda wa kushiriki katika michezo na mashindano dhidi ya shule zingine kutokana na utovu wa nidhamu wakati wa michuano. Unaamini kwamba uamuzi huu utaathiri afya ya wanafunzi. Kama mwakilishi wa shule, mwandikie mwalimu mkuu barua ili uamuzi huu ubadilishwe. Eleza sababu za umuhimu wa kuendelea na utaratibu kamili wa michezo na upendekeze namna ya kuboresha tabia za wanafunzi wakati wa michuano.

### **4. Burudani**

Rafiki wako anaenda kuandaa sherehe ya mwisho wa mwaka wa shule wakati wazazi wake hawapo nyumbani. Kama mwanafunzi ambaye amewahi kushiriki sherehe kadhaa ambazo wazazi hawakuwapo, mwandikie rafiki wako barua-pepe ukimtaadharisha hatari za tukio kama hili na umshauri namna ya kuepukana na shida.

### **5. Sayansi na teknolojia**

Mwalimu wako amekupa mada, "Kitaaluma ni kamili lakini kimadili ni unyama". Kama mwanachama wa klabu ya sayansi shulenii mwako, umeulizwa kutoa hotuba katika gwaride la shule ukiunga mkono au kupinga ukitafakari kuhusu kutumbisha na kuzalisha kwa chupa/uhimilishaji bandia. Andika hotuba yako.

**SEHEMU B**

*Kulingana na kichocheo kifuatacho, toa jibu lako binafsi na ulithibitishe. Chagua maandiko yoyote uliyoyasoma darasani. Andika maneno kati ya 150 na 250.*

6. Vyakula vinavyoundwa kupitia kwa teknolojia ya kisasa vina manufaa katika maisha ya binadamu ingawa madhara yake ni makuu hasa kwa vijana wa sasa.
-